
TAFAKARI ZANGU KUHUSU

# Nehemia 1




JAMES KALEKWA

# TAKARI ZANGU JUU YA NEHEMIA.

James Kalekwa

## Maombi na Mipango

Mwezi Kisleu (Nehemia 1:1) ambapo Nehemia alipashwa habari juu ya watu wa uhamisho,

waliosalia, watu wa nyumbani kwao na habari za mji wa Yerusalemu, mji wake wa wakati wote.

Alijulishwa ni kwamba:

*"Wakaniambia, Watu wa uhamisho, waliosalia huko katika wilaya ile, wamo katika hali ya dhiki nyingi na mashutumu; tena ukuta wa Yerusalemu umebomolewa, na malango yake yameteketezwa kwa moto."*
**Nehemia 1:3**

Mwitikio wa Nehemia ulikuwa wa kihisia na kiroho... hatimaye twajua ALIOMBA!

*"...kisha nikafunga, nikaomba mbele za Mungu wa mbinguni;"*
**Nehemia 1:4**

Siyo tu anasimulia kwamba aliomba bali kuanzia mstari 5-11 (sura yote ya kwanza) tunaona aliomba nini - yaliyomo maombini mwake!

"Baada tu ya maombi" tunatokeza mwezi wa Nisani.

Mwezi wa Kisleu ni sawa na kati ya mwezi Novemba au Desemba kwa kalenda tunayotumia sasa; na mwezi wa Nisani ni sawa na mwezi Machi au Aprili kwa kalenda yetu sasa.

Hivyo tukisema aliomba kuanzia Novemba mpaka Machi AU Desemba mpaka Aprili ni sawa kabisa. Yaani, vyovyote vile, aliomba miezi 5 juu ya ajenda ileile.
Fikiria, miezi mitano unaombea jambo moja!
Inapaswa kuwa hivyo!

Na ghafla mlango unamfungukia mbele yake. Mfalme anahoji na kutaka kuombwa jambo *"...una haja gani unayotaka kumuomba?..."* **Nehemia 2:4**

Baada ya Nehemia kuufunua uhitaji *"... kwani uso wangu usiwe na huzuni, iwapo mji, ulio mahali pa makaburi ya baba zangu, unakaa ukiwa, na malango yake yameteketezwa kwa moto?"*
**Nehemia 2:3**

Haishii hapo, anasema na JAWABU la *uhitaji "Nikamwambia mfalme, Mfalme akiona vema, na ikiwa mimi, mtumishi wako, nimepata kibali machoni pako, tafadhali unipeleke mpaka Yuda, niuendee mji wa makaburi ya baba zangu, nipate kuujenga."*
**Nehemia 2:5**

Hii inatupa kugundua ya kwamba si tu alikuwa anaomba kwa miezi mitano. Vilevile, alikuwa

anapokea majibu mahususi na wajibu wake maalum kwenye utekelezaji wa majibu hayo.

Na baada ya mfalme kuuliza juu ya mpango wa utekelezaji, Nehemia anasema

*"Mfalme akaniuliza, (malkia naye ameketi karibu naye), Safari yako itakuwa ya siku ngapi? Nawe utarudi lini? Hivyo mfalme akaona vema kunipeleka; NAMI NIKAMPA MUDA."*
**Nehemia 2:6**

Haishii hapo, anaomba nyaraka za mfalme kuonyesha kwa maliwali wa ng'ambo na kwa Asafu mlinzi wa mwitu wa mfalme.

Utagundua, Nehemia ana taarifa nyingi sana za safari yake, kazi anayoenda kufanya, na jukumu lake binafsi kwenye hiyo kazi kubwa. Siyo muombaji mtupu; Si mwombaji aisye na ufahamu. Anayajua majibu ya maombi yake kwa yakini.

Alivipata wapi? Ni kwenye maombi!

Kumbe wakati anaomba vilevile alivuviwa kuandaa mpangokazi. Si ajabu mlango ulipomfungikia hakupigwa bumbuwazi/butwaa. Alikuwa na majibu mkononi mwake yaliyokuwa yanasubiri muda uwadie kuyawasilisha kwa ajili ya utekekelezaji.

Kilichounganisha yale maombi na mlango-wazi mbele yake ni mpango.

Ninakuomba kwa BWANA akupe neema ya kusikia taarifa mahususi na mambo maalum ya wewe kufanya.

Ninakuombea ya kwanza BWANA atakupa neema kuandika mpango uliovuviwa na maombi.

Katika Jina la Yesu Kristo!

## Muwako wa hasira za kiongozi

Ujenzi wa ukuta wa Yerusalemu unaendelea; ukombozi wa maisha ya watu walio kwenye hali ya dhiki na mashutumu unaendelea. Maadui kutoka nje wanashindwa... halafu ghafla, mgomo... maandamano... wajenzi wa ukuta na familia zao wanasema kuendelea na ujenzi.

*"Ndipo kukatokea kilio kikuu cha watu, na wake zao, juu ya ndugu zao Wayahudi."*
**Nehemia 5:1**

Na sababu ya mgomo ni *"...juu ya ndugu zao Wayahudi."*

Huu ni ugomvi wa kimfumo ndani ya ukuta unaojengwa. Si mgomo kutokea nje au kutokea kwa maadui wa nje.

Mstari wa 3-6 unafunua kwa maelezo ya ndani kilichokuwa kinaendelea kimfumo baina ya matabaka yaliyounda jamii ya Wayahudi. Uonevu, dhuluma, kodi na utumwa. Mambo haya yalifanywa na ndugu dhidi ya ndugu zao. Hili sitalifjadili kwa upana wake kwenye andiko hili.

Hapa, nimekusudia uone mwitikio wa kiongozi baada ya kazi ya ujenzi wa ukuta kusimamishwa na mgomo wa ndani kwa ndani.

*"Nami nilikasirika sana, niliposikia kilio chao, na maneno hayo."*
**Nehemia 5:6**

Nehemia amebeba picha kubwa ya ukombozi na ujenzi wa ukuta wa Yerusalemu akitokea Ikulu ya Shushani, ngomeni akifanya kazi ya unyweshaji. Alikuwa mtu wa hadhi kubwa. Lakini ameyaacha yote hayo, akaingia kwenye maombi ya kufunga na baadaye akasafiri umbali mrefu kiasi hiki kuwasaidia watu wenye uhitaji kweli kweli. Halafu "wanufaika" wanagoma... wanaleta vilio vikuu. Wanagoma wao na familia zao.

Alikasirishwa na matendo na maneno yao!

Imewahi kukutokea? Watu ambao umetumwa kuwasaidia wanageuka na kuikwamisha kazi (kwa sababu ya tofauti zao ndani kwa ndani).

Imaumiza?

Inavunja moyo?

Inakatisha tamaa?

Inakera?

Ndiyo... Inakasirisha sana.

Sasa, ni vizuri kujua ya kwamba kukasirika ni jambo moja lakini namna ya kushughulika na hasira ni jambo jingine. Kiongozi akikasirika tena akiwakasirikia wanufaika wa uongozi wake... unaelewa madhara yake? Hasira ya kiongozi ni hasara kwa taifa.

Si ajabu Nehemia hakuishia hapo tu. Alipokasirika, hakuchukua hatua kwanza bali...*"Ndipo nikafanya shauri na nafsi yangu..."*
**Nehemia 5:7a**

Ni maombi yangu kwa BWANA ya kwamba utapokea uwezesho wa kuwaza mara mbili kila unapoingia kwenye hali hasira.

Ninakuombea kwa Yesu Kristo akupe utulivu
wa kuweza kutafakari kabla ya kufanya maamuzi kila niingiapo kwenye mtego wa hasira.

Neema ya Kristo Yesu ikusaidie usifanye maamuzi yatakayoathiri na kuleta madhara kwenye maisha ya watu wengi kwa sababu ya hasira zako.

## Sihudhurii vikao vinavyopoteza muda

Ujenzi wa ukuta wa Yerusalemu unaendelea; Utume unaendelea...

Halafu maadui wa kazi ya Mungu, ghafla wanajitokeza tena na kuitisha vikao.

*"Sanbalati na Geshemu wakatuma wajumbe kwangu, wakasema, Njoo, tukutane huko vijijini katika nchi tambarare ya Ono. Walakini wakakusudi kunifanyia mabaya."*
**Nehemia 6:2**

Ukisoma ndani ya mstari huo utaona mwaliko wa kikao na NIA ya kikao. Japokuwa, watoa mwaliko hawakuisema nia yao waziwazi; Nehemia ilipambanua (discern) nia ovu waliyokuwa nayo dhidi yake kama kiongozi... *"wakakusudia kunifanyia mabaya."*

Baada ya mtu wa Mungu kupambanua nia yao anajibu kwa maneno makubwa sana:

*"Na mimi nikatuma wajumbe kwao, nikasema, Hii ni kazi kubwa ninayoifanya mimi, hata nisiweze kushuka; mbona kazi ikome, hapo ninapoiacha, niwashukie?"* **Nehemia 6:3**

Kwa ulinganifu (comparatively), kazi ya Mungu niifanyayo... wito ninaokimbizana nao... matokeo ninayohimizwa kuyazalisha ni MAKUBWA mno kuliko hivyo vikao. MBONA KAZI IKOME? Kisa na mkasa ni nini?

Hii kazi ni kubwa ninayoifanya mimi!!!

Ni kama anajivuna;

Kama amejaa dharau;

Kama hapendi mahusiano na watu;

Ukweli ni kwamba "HII KAZI NI KUBWA MNO." Ni kujitambua tu. Ni vizuri ukiwa kwenye nafasi ya uongozi ujue ukubwa wa kazi uliyopewa.

Kwa mfano, familia yako, yaani, mke wako na watu wa nyumbani mwako ni kazi kubwa mno. Usiififishe au kuizamisha kisa vikao na akina Sanbalati na Geshemu.

Hata hivyo, hawa maadui hawakuchoka.

*"Nao wakaniletea maneno kama hayo mara nne; nikawajibu maneno kama yale."*
**Nehemia 6:4**

Hebu fikiria... kadi nne za mwaliko; SMS nne za mwaliko; simu nne za mwaliko; barua nne za mwaliko... vyovyote vile - alialikwa mara nne! Unaweza kukataa mara ya kwanza, na ya pili... lakini hizi zingine kwa sababu ya aibu, au kuwaogopa watu unaamua kukubali tu!

Sivyo ilivyokuwa kwa Nehemia. Ndiyo yake ni ndiyo na hapana yake ni hapana!

Kuna utume ambao umeubeba na leo kuna kipande cha utume unapaswa kutimiliza. Kuna mambo ambayo unapaswa kuzalisha matokeo leo!!?

Siyo tu ninakuombea uwaepuke akina Sanbalati na Geshemu, bali uwe makini ya kwamba wewe usiwe Sanbalati wako mwenyewe... Usijipe vikao vyenye nia ya kukutenda mabaya.

Inagharimu moyo unaopambanua (discernment) kujua kikao cha kwenda na cha kutokwenda.

Ninakuombea neema ya Yesu Kristo na uwezesho wa Roho Mtakatifu uweze kupambanua vikao na nia zake sawasawa.

Ninamuomba Roho Mtakatifu akuwezeshe kwamba usiangukie kwenye mtegoo wa kuwaogopa wanadamu au kuona aibu.

Mungu akupe neema ya kusema ndiyo na /au hapana na kubaki hapo.

Katika Jina la Yesu Kristo!

## Watesi hunyenyekezwa kwa kuzalisha matokeo:

Iwe unajua au haujui; unataka au hautaki; unapenda au haupendi... kwenye maisha kuna watesi. Watu ambao hawafurahii "Ujenzi wa ukuta wa Yerusalemu na kuwaondoa watu kwenye hali dhiki na mashutumu." Watu ambao pengine bila hata sababu wanachukizwa na utumishi uliobeba; hawapendi uelewa wako; hawapendi namna unayoitumia kufanya jambo husika. Na watesi hawa wanachukulia

ulifanyalo kiasi kwamba wangetamani ukwame au wewe na hiyo kazi mfutike kabisa.

Unamkumbuka Sanbalati na Geshemu?

Kwani, Nehemia alifanya nini ili *"kujipatia"* uadui toka kwao?

Na kuna wengine inawezekana unaleta madhara kwenye maslahi yako ya wazi au ya sirini kwa namna fulani.

Na wengine wanatishwa (intimidated) na wewe. Wanakuona kama adui.

Hawa watu watajaribu kila namna kujaribu kukutoa kwenye mstari.

1. Watadhihaki unachokifanya na kukidunisha kionekane si lolote si chochote *"Lakini waliposikia Sanbalati, Mhoroni, na Tobia, mtumishi wake, Mwamoni, na Geshemu, Mwarabu, walitucheka, wakatudharau, wakasema, Ni nini neno hili mnalofanya? Je! Mtaasi ninyi juu ya mfalme?"* Nehemia 2:19

2. Watajaribu kuwavunja "watu wako" nguvu. Wakikushindwa wewe, wataliendea kundi "Lakini ikawa, Sanbalati aliposikia ya kwamba

tulikuwa tukiujenga ukuta, akaghadhibika, akaingiwa na uchungu sana, akawadhihaki Wayahudi." Nehemia 4:1

3. Watakuita kwenye vikao vinavyopoteza muda (time wasters) - **Nehemia 6:2-5**

4. Watatoa unabii feki ili kukupandikizia hofu; watatunga maneno ya uongo (conspiracy) - *"Nikatambua, na tazama, siye Mungu aliyemtuma; lakini amefanya unabii huu kinyume changu; nao Tobia na Sanbalati ndio waliomwajiri 13 Kwa sababu hii aliajiriwa, ili mimi niogope, nikafanye hivyo na kutenda dhambi, kisha wao wawe nazo habari mbaya, ili wanishutumie."* **Nehemia 6:13**

Usijaribu kuingia mtego wa malumbano, mashindano, majibizano... usingie mtego huo! Mashindano ya maneno hayana faida! Tena, ukishindana nao anafanana nao.

Jielekeze kwenye kazi yako uliyoitiwa. Jikite kwenye utume wako. Kitu pekee kitakachowanyenyekeza ni MATOKEO na si maneno matupu.

*"Ikawa adui zetu wote waliposikia, ndipo makafiri wote waliotuzunguka wakaogopa, nao wakakata tamaa sana machoni pao wenyewe; maana waliitambua kazi hiyo ilivyotendwa na Mungu wetu."* **Nehemia 6:16**

Punguza mijadala.

Punguza mabishano.

Punguza mashindano ya maneno.

ZALISHA MATOKEO!!!

Mungu akupe neema ya kupunguza mdomo na maneno na kuongeza juhudi ya kazi na kuzalisha matokeo kwa Jina la Yesu Kristo!

## Nyuma ya Takwimu ni watu na maisha yao halisi – wafahamu!

(Nehemia Sura ya 7)

Kuna wakati nimewahi kumasikia Mzee Derek Prince akifafanusha kuhusi kutotanguka hata yodi na nukta mona ya maandiko. Hiyo ilinipa kuliendea neno la Mungu kwa kujua ya kwamba si tu aya au sentensi bali alama zote ndani yake zina maana kubwa.

Sura ya saba ya Nehemia, ujenzi wa ukuta umekamilika kuna ukurasa mwingine wa maisha unafunguka.

*"Mungu wangu akanitia moyoni mwangu, kwamba niwakusanye wakuu na mashehe, na watu, ili wahesabiwe kwa nasaba. Nikakiona kitabu cha vizazi vya hao waliokwea hapo kwanza, nikaona ya kwamba imeandikwa humo;"*
**Nehemia 7:5**

Nehemia anakusanya viongozi (wakuu na mashehe) na kutoa maelekezo ya watu kuhesabiwa, tafsiri za kiingereza zinasema kuorodheshwa/kuandikishwa kwa nasaba... kumbe mkazo hauko kupata orodha tu ya watu. Ingeweza kupatikana vyovyote vile; mkazo upo kwenye namna watu wanapaswa kuorodheshwa... kwa NASABA! Kwa familia, kwa ukoo, kwa kufahamu chimbuko la mtu mmoja mmoja.

Niliposoma hapa, nikakumbuka kwenye Agano Jipya, namna Yesu alivyozaliwa. Ni amri ilitoka kwa Kaisari Augusto ya kuandika majina (kuhesabiwa) kila mtu nyumbani kwao (Luka 2:1-3).

Kilichovuta umakini wangu ni kwamba jambo lilivuviwa moyoni mwa Nehemia na MUNGU mwenyewe. Siyo tu kwamba ni wazo zuri, bali ni

wazo la Mungu (It is not merely a good idea, it's a God's idea)!

Kwa utulivu nikafahamu ya kwamba Mungu amekusudia Nehemia asiwe kiongozi anayewajua watu kwa takwimu tu. Angeweza kufanya hivyo, na idadi ya watu - wanawake, wanaume, watoto, makundirika- bado angepata idadi ileile. Na kumbe mkazo wa Mungu uko kwenye NASABA! Kuwafahamu watu na maisha yao halisi. Kuwafahamu watu kwa undani wao na si juu juu.

Unakumbuka habari ya Gideoni ambaye alisalimiwa na malaika kwa utambulisho wa *"Ee, shujaa"* (Waamuzi 6:12). Lakini Gideoni alikaza kujitambulisha kwa uduni wake kwa sababu ya NASABA (Waamuzi 6:15) - nyumba ya baba yake, jamaa zake kisha kabila lake la Manase!?

Kumbe ili uwahudumie watu ni vizuri kuwafahamu zaidi ya takwimu zinazowasilishwa kwenye karatasi. Ni kweli kwenye hilo eneo kunaweza kuwa na wanaume 20. Lakini 20 haitoshei kuwaelezea vyema. Kila mtu ni mtu binafsi; ni mtu halisi na ana maisha halisi. Kila mwanaume kwa hao 20 ana simulizi, shuhuda, changamoto, ushindi, uelekeo... na kwa ujumla wake ana MAISHA!

Usisahau wito wa utumishi wa Nehemia ulianzia hapa:

*"Hanani, mmoja wa ndugu zangu, akanijia, yeye na watu wengine waliotoka Yuda; nami nikawauliza habari za Wayahudi waliopona, hao watu wa uhamisho waliosalia; na habari za Yerusalemu."* **Nehemia 1:2**

Aliguswa sana kufahamu habari za WATU na habari za MJI.

Kwa habari za MJI alijibiwa ya kwamba, *"... tena ukuta wa Yerusalemu umebomolewa, na malango yake yameteketezwa kwa moto."* **Nehemia 1:3b**

Na kwa habari za WATU alijibiwa *"...wakaniambia, Watu wa uhamisho, waliosalia huko katika wilaya ile, wamo katika hali ya dhiki nyingi na mashutumu..."*

Na kwenye sura hii hapa Nehemia amemaliza nusu ya maishani yake. Ujenzi wa ukuta. Kipande cha pili ni maisha ya watu. Na asingeweza kuwahudumia itakikanavyo watu asiowafahamu kinagaubaga.

Swali likaniijia: Je, ninawafahamu kiasi gani watu wangu?

Je, unamfahamu kiasi gani mwenzi wako? Watoto wako? Kundi lako? Washirika wako? Wafanyakazi wako?

Mzee John Maxwell ameandika mara kadhaa "*Watu hawajali ni kiasi gani unajua, bali ni kiasi gani*

*unajali." (People do not care how much you know, but how much you care.)*

Mungu akupe neema, bidii na moyo wa KUWAJUA watu wako ili uwaongoze.

## Watu wote kama mtu mmoja

(Nehemia sura ya 8)

Shughuli ya ujenzi wa ukuta wa Yerusalemu imekamilika; Sasa shughuli ya ujenzi wa watu na maisha yao inaanza... ujenzi wa watu ulianza kwenye sura ya saba kwa kuchukua takwimu za watu - kuwafahamu watu kitakwimu lakini zaidi kwa nasaba/mbari (koo) zao.

Ilikuwa hivi,

Watu wamegawanya kwenye makabila, kisha kutoka kwenye makabila wakagawanywa kwenye koo/mbari/nasaba zao na kutokea hapo watu wakagawanywa kwenye ngazi ya familia. Huu mgawanyo ni kama jeshini- kundi kubwa linavunjwa mpaka kuwa kundi dogo linaloeleweka!

Ingeweza kuonekana ni ukabila; ni kuwatenga watu; ni kuwasababisha watu wawe mbali mbali zaidi. Asante Yesu kwamba habari haikuishia hapo.

*"Na watu wote wakakusanyika kama mtu mmoja katika uwanja uliokuwa mbele ya lango la maji;*

*wakamwambia Ezra, mwandishi, akilete kitabu cha torati ya Musa, Bwana aliyowaamuru Israeli."*
**Nehemia 8:1**

Watu wote - maana yake ni watu wote; rika zote, waume kwa wake; wakubwa kwa wadogo; kabila zote, koo zote, familia zote... watu wote!!!

Watu wote wakakusanyika. Yaani baada ya kugawanywa ili kuhesabiwa, kuna kuja pamoja. Lakini sasa hivi si tu kwamba wamekusanyika bali kuna sifa ya kusanyiko... KAMA MTU MMOJA!

Yaani, ukilitazama kusanyiko huoni tena tofauti zao zikitokeza kwa nguvu kuliko kinachowaunganisha. Wanaume na wanawake ni kama mtu mmoja; makundirika tofauti ni kama mtu mmoja - huwezi tena kuchora mstari baina ya wazee, watoto na vijana; kabila zote na koo na familia zote ni kama mtu mmoja - huwezi kuona tofauti yao!

Si kwamba makabila yamepotea; si kwamba koo zimefutwa; si kwamba familia hazipo;

Ni kweli kwamba waliendelea kuwa na umri tofauti, jinsia tofauti... walikuwa tofauti.

Hata hivyo, kulikuwa na kitu kikubwa na cha thamani sana kiliwaleta pamoja kuliko jambo lolote linalowatofautisha. Walichukuliwa sana na jambo hilo kubwa kiasi kwamba tofauti zao zikafifia.

Kumbe kuna jambo (maono) huwakusanya watu na kuwafanya kuwa mtu mmoja.

Kumbe uwepo wa tofauti si tatizo; tofauti zinaanza kuwa au kuleta tatizo pale ambapo hakuna maono yanayounganisha.

Mzaburi husema,

*"Tazama, jinsi ilivyo vema, na kupendeza, Ndugu wakae pamoja, kwa umoja."*
**Zaburi 133:1**

Na kwa hakika hatua kubwa zaidi ambayo tumekusudiwa kuifikia kama jumuiya ya waamini ni UMOJA WA IMANI!

*"hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo;"*
**Waefeso 4:13**

Yesu lisaidie kanisa lako la mahala pamoja kuwa kusanyiko la "WATU WOTE KAMA MTU MMOJA."

Roho Mtakatifu liwezeshe kanisa lako la Tanzania kuwa "WATU WOTE KAMA MTU MMOJA."

Katika Jina la Yesu Kristo!

## Kitabu – Mwanzo, Mwisho!

(Nehemia sura ya 8)

Ujenzi wa ukuta wa Yerusalemu umemalizika; ujenzi wa watu ndani ya kuta unaanza.

Na mwanzoni kabisa mwa ujenzi wa watu tunakutana na matumizi ya KITABU...

*“Naye Ezra, kuhani, akaileta torati mbele ya kusanyiko, la wanaume na wanawake, na wote walioweza kusikia na kufahamu, siku ya kwanza na mwezi wa saba.”*
**Nehemia 8:2**

Mstari unaofuata tunaona alisoma "humo" yaani kutokea kwenye KITABU (torati). Na baadaye tunaona

*"Ezra akakifunua kitabu machoni pa watu wote; (maana alikuwa juu ya watu wote); na hapo alipokifungua, watu wote walisimama;"*
**Nehemia 8:5**

Ninavutwa sana na mwitikio wa watu pale kitabu kinapofunuliwa na kuhani, Ezra... ninajaribu kutengeneza taswira mawazoni mwangu, kuliona lile kusanyiko linavyoinuka baada ya kuona KITABU kinafunuliwa.

Fikiria namna hii, kama umewahi kuhudhuria makusanyiko yanayozingatia itifaki; Hususani itifaki iliyokazwa sana. Utakubaliana na mimi ya kwamba mtu anayeheshimiwa sana au mkuu kiitifaki kwenye kusanyiko husika anapowasili au anapotoka watu husimama juu kama ishara ya heshima au kuitambua nafasi ya mtu husika. Kwenye kusanyiko mchanganyiko, mwongozaji wa husema *"sasa tusimame, tumpokee XYZ..."* Lakini kwenye kusanyiko lililofundwa kiitifaki mpaka ikawa ni maisha yao, hujikuta wamesimama tu bila kutangaziwa.

Sasa, fikiria kusanyiko hili la ibada linainuka juu, kama kusanyiko lililofundwa itifaki, kwa ajili ya KITABU... heshima ya kitabu; nafasi ya kitabu; uzito wa kitabu; upekee wa kitabu... KITABU ndiye mgeni wa heshima na mgeni mashuhuri!

Ona kitabu kinavyopewa heshima...

*"Ezra akamhimidi Bwana, Mungu Mkuu. Nao watu wote wakaitika, Amina, Amina, pamoja na kuinua mikono yao; kisha wakainama vichwa vyao, wakamsujudu Bwana kifudifudi."*
**Nehemia 8:6**

Amina!

Amina!

Iwe hivyo; Iwe hivyo

Halafu wakainua mikono; kisha wakainama na kusujudu.

Uchaji wa hali ya juu sana kwa KITABU!

Hapo hata hakuna ufafanuzi wa jambo lolote; ni kusoma tu... mwitikio wa ajabu namna hii.

Baadaye kukawa na timu ya watu waliofafanusha maneno ya KITABU kiasi cha watu kuyafahamu yaliyosomwa (mstari 8)

*"Naye Nehemia, ndiye aliyekuwa Tirshatha, na Ezra kuhani, mwandishi, na Walawi waliowafundisha watu, wakawaambia watu wote, Siku hii ni takatifu kwa Bwana, Mungu wenu; msiomboleze wala msilie. Maana watu wote walilia, walipoyasikia maneno ya torati."* **Nehemia 8:9**

Mwishoni mwa mstari wa 9 unaona mwitikio mwingine. Baada ya watu kuelewa ufafanuzi, wanaitikia kwa maombolezo na vilio...

Inawezekana walikuwa na muda mrefu sana hawajalisikia neno la Mungu; au hawajasikia uzito/mkazo wa namna hii wa neno; au walishangaa kuona "walifinyiliwa kiasi gani" kumbe walipaswa kufaidi na hawakujua.

KITABU kikazalisha aina fulani ya furaha ya Mungu ndani ya mioyo ya watu. Wanafanya furaha nyingi, wakala na kunywa kwa sababu KITABU kilikuwa kimeeleweka kwao... kwa kadiri kusanyiko linavyokielewa KITABU utaona aina fulani ya furaha/changamko linazaliwa.

Utagundua FURAHA ni matokeo ambayo yanasemwa karibia kila mstari wa sura hii. Kwamba KITABU kimezalisha furaha miongoni mwa watu.

Kusanyiko hili la kusoma KITABU liliendelea kwa siku saba... ni kama kambi fulani hivi, ambapo ni mwendo wa KITABU tu asubuhi, mchana na jioni; KITABU mwanzo, mwisho!

Kuanzia mwanzo wa sura hii KITABU kinatawala kusanyiko.

Na huo ndo mwanzo wa ujenzi wa watu ulivyoanza... KITABU!

Ninakuombea kwa Yesu wewe uwe ni moja ya watu watakaokipa KITABU heshima yake ya juu!

Ninamuomba Mungu akupe mwitikio wa heshima ya hali ya juu kila usikiapo maneno ya KITABU.

Kila lisomwapo neno la Mungu, furaha
yako iongezeke katika Jina la Yesu Kristo!

## Je, mtu kama mimi nikimbie?

(Nehemia sura ya 6)

Baba yangu wa kiroho, Pastor Goodluck Kyara, amewahi kutufundisha hivi (ninaweza nisurdie neno kwa neno).

*"Kujitambua si kujivuna; kujidunisha si unyenyekevu. Ni uneyenyeku sana kujitambua wewe ni nani na wewe si nani." Pastor Goodluck Kyara*

Wakati ninaendelea kujifunza kutokea kwenye kitabu cha Nehemia, ujenzi wa ukuta wa Yerusalemu unaendelea. Ghafla nikakutana na maneno makali namna hii kutoka kwenye kinywa cha mtumishi wa Mungu. Ni maneno ya kibabe sana...

*"Nami nikasema, Je! Mtu kama mimi nikimbie? Naye ni nani, akiwa kama nilivyo mimi, atakayeingia hekaluni ili kuponya maisha yake? Sitaingia."*
**Nehemia 6:11**

Ni kweli kukimbia ni njia mojawapo ya kujiokoa dhidi ya mashambulizi;

Ni kweli mambo yakizidi Luna watu hukimbia;

Ni kweli unaweza kukimbilia hekaluni kuponya maisha yako.

LAKINI kuna watu na watu... mtu kama mimi... HAPANA! Watu wa namna hii huwa wanakutana na changamoto uso kwa uso, na changamoto huwa zinayeyuka zenyewe.

Anaposema mtu kama mimi, lazima tumwelewe vyema.

1. Ni mtu wa magotini sana (Nehemia 1:5-11) unaona anavyojimwaga kwenye maombi. Aina hii ya mtu, tumaini lake ni Mungu. Usicheze naye! Ni vizuri ujue anayepiga magoti sana, husimama sana.

2. Ni mtu aliyeacha vyote kwa ajili hii (Alikuwa mnyeshaji wa mfalme mkubwa wa zama hizo huko Shushani, ngomeni) - ukiacha vyote, huna tena cha kupoteza.

3. Afadhali ufe ukipambania hiki kuliko kufa kama coward (Nehemia 1&2)

4. Kiongozi jawabu la hitaji la wakati (man of the hour) - hawa ni wale wanaoujia ufalme kwa wakati kama huu. Hakukuwa na mtu mwingine mwenye ujasiri kujenga ukuta na kuwasaidia watu wa Yerusalemu. Nehemia ni mtu wa saa hii! Anajua kwa yakini kwamba yeye akikimbia, hakuna atakayesimama.

5. Mtu wa kimkakati [strategic]; pamoja na alichokibeba lakini hafanyi mambo kiholela. Angalia alivyoi mbele ya mfalme na baadaye kupewa kibali ALITOA MUDA (Nehemia 2:6) - alitoa "timeframe" na baadaye aliendelea kuomba rasilimali, nyaraka na ulinzi ili maombi yake yasikwame kwa kutojua itifaki za kuiingia miji (Nehemia 2:7-9); na hata alipoingia Yerusalemu aliendа kimkakati sana (Nehemia 2:11-19).. angalia mpangilio na mtiririko wa kazi ya ujenzi wa ukuta (Nehemia 3). Huyu ni strategic leader. Si mtu wa kukurupuka!

Anaposema mtu kama mimi, anarejelea *"vinasaba"* vya uongozi vinavyomuunda yeye!

Sasa, mtu wa namna hii anakimbiaje? Anakimbia ili iweje?

Ni kweli mashambulizi yalikuwa halisi mbele yake. Ukisoma:

*"Nikaingia nyumbani kwa Shemaya, mwana wa Delaya, mwana wa Mehetabeli, aliyekuwa amefungwa; naye akasema, Tukutane nyumbani mwa Mungu, ndani ya hekalu, tukaifunge milango ya hekalu; kwa maana watakuja kukuua; naam, wakati wa usiku watakuja kukuua."*
**Nehemia 6:10**

Watakuja kukuua!

Watakuja kukuua!

Hii ni sentensi imerudiwa mara mbili na Shemaya akimmegea siri Nehemia. Na akaandaa mpango wa kumnusuru kutoka kwenye mauaji hayo.

Iwe iwavyo, iwe jua ama mvua... mtu kama mimi sikimbii.

Napenda sana pale Nehemia anapotoa hitimisho fupi lakini la ujasiri wa kiungu kwa kusema "SITAINGIA"

Nami nakuuliza leo,

mtu kama wewe ni wa kuacha hiyo ndoa?

Mtu kama wewe ni wa kuishia kwenye talaka?

Mtu kama wewe ni wa kukimbia huduma?

Mtu kama wewe ni wa kukimbia biashara?

Mtu kama wewe ni wa kuzika hiyo ndoto?

Mungu akupe neema ya kusema "SITAKIMBIA"

Ikabili changamoto yako.

Mtu kama wewe si wa kukimbia!

## Kuhusu Mwandishi:

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis “Tai”, Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *“Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.”* [Habakuki 2:14]

## Kuhusu New Vine Church:

Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

## Mawasiliano na Mwandishi:

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi n audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: James Kalekwa

Instagram: james_kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-7764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

# KUHUSU MWANDISHI



**James Kalekwa** ni amemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma.


James Kalekwa

james_kalekwa

@MchungajiJK

+255 754 917 764